

MJASILIAMALI NI MHANGAIKAJI

Zifahamu tabia za mjasiliamali na
utengenezaji wa bidhaa

Na Patrick Y.Sikayinda

1. HUJIULIZA MASWALI YA MSINGI.

Bill Gates alisema, *“Umezaliwa maskini siyo kosa lako, lakini ukifa maskini ni kosa lako,”*

Mjasiliamali lazima ajiulize:-

Je nina ujuzi wa kufanya biashra hii?

Je nikajifunze wapi ujuzi ninaohitaji?

Je ni wazo gani ninaweza kuligeuza kuwa chanzo cha kupata kupato?

Je bidhaa hii wateja wanaihitaji?

Je wateja wangu wana uwezo gani wa kununua?

Hili eneo ambalo ninataka kuweka biashara linapitiwa na wateja ?

Je bidhaa zitawafikiaje wateja wangu?

Je wateja wangu wana imani zipi?

Je wateja wangu wana tabia zipi?

Je umewahi kujiuliza maswali haya? Na mengine mingi. Unayaonaje si yanakupa hisia fulani eti? Maswali haya ni ya msingi sana.

Ili usije ukaweka bidhaa mahali ambapo wateja ni wachache sana au uwezo wao wa kununua ni mdogo au hawazihitaji bidhaa zenyewe ulizowaletea

Hivyo gharama za kuendeshea biashara zikawa kubwa kuliko faida inayopatikana baada ya mauzo.

Lakini pia unaweza kuweka bidhaa ambazo wateja wako hawawezi kumudu bei zake.

Watu wengi huwa hawajiulizi maswali haya na mengine mengi halafu huanza biashara mahali ambapo biashara haikui na hivyo hufanya biashara kwa kitambo tu na baada ya fedha ya pango kuisha huwa hawawezi kuendelea. Nao huishia pale pale.

Hivyo biashara nyingi hufa baada ya miaka miwili hadi mitano. Fanya utafiti kabla ya kujiingiza kwenye ujasiliamali, wengi hufanya ili waonekana kuwa nao wana biashara kitu ambacho husababisha hasara kubwa na mashaka. Kumbuka ulivyojinyima ili kupata mtaji wenyewe. Hivyo usianzishe biashara ili mradi watu wakuone na wewe una biashara ,tulia, jiulize maswali ya msingi na yapatie majibu sahihi.

2. WANA HAMASA BINAFSI

***“Nilijua kuwa kama nikifeli sitajutia kwa hilo,lakini nilijua kitu kimoja ninachuweza kukijutia ni kutokujaribu.”*Jeff Benzos mwanzilishi wa Amazon.**

Kumbuka kuanza ni rahisi lakini kuendelea kujihamasisha na kuendeleza moto ule ule wa mwanzoni nayo ni changamoto sana. Na lazima ujiendeshe kwa ari ile ile ya kwa nini ulianza. Wajasiliamali wapo tayari kuendelea kuhangaika na kuvumilia mpaka kufika kwenye mafanikio.

Na huendeleza uvumilivu, pia hii ni moja ya sifa inayoweza kuwatenganisha waliofanikiwa na wasiofanikiwa. Wapo tayari kila iitwayo siku kufanya kazi masaa mengi, kufanya kazi kwa bidii kwa kujitoasana.

Hiyo ni sifa ambayo na wewe ni lazima uwe nayo kwa vile hakuna atakayekuja kukuhamasiha.

Huanzisha shughuli yoyote kwa kutumia fedha mwanzoni wakiamini zitarudishwa na biashara hiyo.

Wanajihamasisha balaa , wanataka kupata mafanikio na faida. Kumbuka hawa ni mabosi wenyewe hivyo hujiongoza wenyewe. Hawasimamiwi na yeyote bali na wao wenyewe.

Wanapanga muda wa kazi na kupanga matumizi yake wao wenyewe.

Mioyo yao inawaka moto wa kufika mbali. Hawatamani vitu wanavyoviona tu bali husema hivi ni lazima wavipate. Faida ndiyo ambayo huwahamasihsa mno. Wakianguka chini huamka , wakifeli hujifunza,na kamwe huwa hawarudii makosa.Hujiuliza maswali ya msingi na kuyapatia majibu ya maana. Hujisukuma wenyewe, na huendelea kusonga mbele hata kama malipo hayaji leo hii.

Uzuri wa kupata fedha nyingi zitakazomfanya anunue anachotaka, aende anakotaka au awasaidie anaotamani kuwasaidia. Hii ndiyo hamasa kuu kwa wajasiliamali wengi kwa vile wanataka wasiwe wanaishi kwa hofu ya kuishiwa na kukosa uhuru wa kufanya watakacho

Na wewe hiyo ndiyo iwe ni hamasa yako kuu..

3. HUCHUKUA HALI HATARISHI

Usielekeze macho juu ya kwa nini huwezi kufanya kitu kitu ambacho watu wengi hufanya.Unatakiwa kufokasi juu ya kwa nini labda unaweza kuwa miongoni mwa wasio wa kawaida.”Steve Case.

Je unajua maana ya kuchukua hali hatarishi? Ngoja nikueleze maana yake. Maana yake ni kufanya jambo ambalo huna maamuzi asilimia mia juu ya matokeo yake. Kwa mfano unasema nitatumia fedha kiasi fulani kulima eka kumi za mazao fulani. Na unazitumia kweli wakati huna uamuzi na hali ya mvua au kiasi cha mvua itakayokuja msimu huo.

Wewe una imani kuwa mvua ya kufaa itanyesha .

Watu wengi wanaweza kusita kuchukua hali hatarishi kwa vile ni waoga wa kupoteza fedha, wanataka usalama na kutulia kwa starehe nyingi. Hawataki kuonekana wajinga kwa kushindwa. Hawataki kukutana na kukataliwa wala kuchekwa.

Wajasilimali wanajua kuchukua hali hatarishi wakitumia akili nyingi kufikia maamuzi. Kama unataka kuwa mjasilisamali lazima ufahamu kuna kushindwa pia. Na hawajiwekei uwezekano wa kushindwa bali hujitahidi kufanya kila linalowezena na kutumia akili na maarifa mengi kuwawezeshe kupata matunda tarajiwa.